

policy forum

ZIJUE KANUNI ZA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA: NGAZI YA VIJIJI, MITAA NA VITONGOJI, 2019

Kimeandaliwa na:
Kikosi Kazi cha Policy Forum na kuhakikiwa na
Kikundi Kazi cha Tawala Serikali za Mitaa

Mchora Katuni:
Regis Maro

Kimesanifiwa na Kupigwa Chapa na:
Jamana Printers Limited

ISBN: 978-9987-708-37-6

ZIJUE KANUNI ZA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA: NGAZI YA VIJIJI, MITAA NA VITONGOJI, 2019

Yaliyomo

Shukrani 5

1. Utangulizi 6
2. Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, 2019 7
3. Tangazo la Uchaguzi 7
4. Uratibu na Usimamizi wa Uchaguzi 7
5. Maelekezo Kuhusu Uchaguzi 8
6. Makosa ya Uchaguzi na Adhabu Zake 9
7. Uandikishaji wa Wapiga Kura 10
8. Sifa za Mpiga Kura 11
9. Kupoteza Sifa za Kupiga Kura 11
10. Sifa za Mgombea 12
11. Mgombea Kupoteza Sifa 13
12. Uteuzi wa Wagombea (kuchukua na kurejesha fomu) 13
13. Mahali, Vituo na Muda wa Kupiga Kura 14
14. Utambulisho wa Mpiga Kura 14
15. Siku ya Upigaji Kura 15
16. Usaidizi kwa Watu wenye Mahitaji Maalum 16
17. Kuhesabu Kura 16
18. Kutangazwa kwa Matokeo 17
19. Kutobatilisha Matokeo ya Uchaguzi 18
20. Kampeni za Uchaguzi 18
21. Waangalizi wa Ndani wa Uchaguzi 18
22. Elimu ya Mpiga Kura na Uraia 19

Kiambatanisho 1: Kalenda ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2019 20

Shukrani

Shukrani za dhati ziende kwa wajumbe wa kikosi kazi walio andaa andiko hili kwa kuratibiwa na kikundi kazi cha Tawala Serikali za Mitaa cha Policy Forum hususan Kellen Mngoya – HAFOTA, Hebron Mwakagenda – The Leadership Forum, Israel Ilunde – YPC, Deus Kibamba – Tanzania Citizens' Information Bureau/USHIRIKI Tanzania, Goodluck William Minja- UNA Tanzania, William Mtwazi – LHRC, Rehema Maro – WILDAF/USHIRIKI Tanzania na Jimmy Luhende – Actions for Democracy and Local Governance (ADLG)

1. Utangulizi

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya 8(1) (a); wananchi ndio chimbuko la mamlaka ya utawala wa nchi na kwamba Serikali itapata mamlaka kutoka kwao. Uchaguzi ndio namna pekee ya wananchi kukasimisha mamlaka yao kwa viongozi. Ni Haki ya kila raia kushiriki katika michakato ya Uchaguzi ikiwemo kupiga au kupigiwa kura kwa mujibu wa Katiba na sheria za nchi ili kupata viongozi. Hivyo ni muhimu Serikali kuhakikisha kwamba wanachi wanapata fursa ya kushiriki katika chaguzi huu wa Serikali za Mitaa, 2019.

Moja ya changamoto ya ushiriki wa wananchi katika chaguzi za Serikali zilizopita ni kukosa au kuchelewa kupata taarifa sahihi na kwa wakati kuhusu Uchaguzi. Sehemu kubwa ya taarifa za Uchaguzi kwa mwaka 2019 zipo kwenye Tangazo la Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji, na Vitongoji namba 371, 372, 373 na 374 ya mwaka 2019 lililowasilishwa na Waziri wa nchi, Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI). Aidha, taarifa zaidi zipo katika ratiba ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambazo ni kiambatanisho katika Tangazo.

Zijue Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ngazi ya Vijiji, Mitaa na Vitongoji*, 2019* ni kijitabu kinachofafanua Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, 2019 kwa lugha rahisi.Hii ni moja ya juhudi za mtandao wa Policy Forum na Mtandao wa Waangalizi wa Uchaguzi Tanzania (TACCEO) za kurahisisha taarifa mbalimbali ili ziwafikie wananchi kwaajili ya kupata uelewa ili kushiriki michakato mbalimbali ya maendeleo.

Tunaamini kuwa kupitia kijitabu hiki Watanzania watapata taarifa za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, 2019 na hivyo kushiriki kikamilifu kwenye Uchaguzi huu hatimaye kuchangia katika Uchaguzi huru na wa haki nchini.

Watakaopata fursa kusoma kijitabu hiki, watapata taarifa muhimu za kimaudhui na kimchakato ikiwemo masuala yanayojitokeza katika Kanuni za Chaguzi wa Serikali za Mitaa pamoja na Ratiba yake.

2. Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, 2019

Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, 2019 utahusisha wananchi kuchagua viongozi katika makundi matatu. Kwa mujibu wa kifungu cha 4 (3) cha Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kutakuwa na Uchaguzi wa Mwenyekiti na wajumbe watano (5) wa kamati ya Mtaa; Mwenyekiti na wajumbe ishirini na tano (25) wa Halmashauri ya Kijijji na Mwenyekiti wa Kitongoji.

Uchaguzi huu unaongozwa na Kanuni zifuatazo:

- Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), 2019 (Sura 287) inayohusu Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji.
- Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji Midogo), 2019 (sura 287) inayohusu Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka Ya Miji Midogo.
- Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), 2019 (Sura 288) inayohusu Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mtaa pamoja na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa.

Uchaguzi utafanyika tarehe **24/11/2019** kwa mujibu wa Tangazo na ratiba ya Uchaguzi kama ilivyotolewa na Waziri mnamo tarehe 23/08/2019 na kusambazwa na vyombo mbalimbali vya habari.

3. Tangazo la Uchaguzi

Tangazo la Uchaguzi linahusu mambo makuu mawili:-

1. Masharti muhimu ya Uchaguzi kwa mujibu wa sheria na Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, 2019
2. Ratiba ya Uchaguzi na shughuli zinazohusika na Uchaguzi.

4. Uratibu na Usimamizi wa Uchaguzi

Ili kuhakikisha kwamba Uchaguzi huu unaratibiwa na kusimamiwa ipasavyo, Kanuni zinawataja Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi na Msimamizi wa Kituo ndio watakaoteuliwa kusimamia Uchaguzi.

Kwa upande mwingine Kanuni zinakataza wafuatao kuteuliwa kuwa waratibu na wasimamizi wa Uchaguzi:-

(a) Kiongozi wa Chama cha Siasa;
(b) Mgombea;
(c) Hakimu au Jaji;
(d) Kiongozi wa Dini;
(e) Askari wa Jeshi lolote;
(f) Katibu Tawala wa Wilaya;
(g) Katibu Tawala wa Mkoa;
(h) Mkuu wa Wilaya na;
(i) Mkuu wa Mkoa.

5. Maelekezo Kuhusu Uchaguzi

Tangazo la Uchaguzi limempa jukumu Msimamizi wa Uchaguzi atakayeteuliwa kutoa Maelekezo ya Uchaguzi siku 62 kabla ya siku ya Uchaguzi. Maelekezo hayo ni:-

(a) Tarehe ya kufanyika kwa Uchaguzi (hii ni tarehe ya kupiga kura);
(b) Muda na sehemu ya kuandikisha wapiga kura;
(c) Muda na mahali pa kupigia kura;
(d) Kuwataka wakazi wote wenye sifa kushiriki Uchaguzi;
(e) Kuwataka wakazi wenye umri wa miaka ishirini na moja (21) au zaidi wanaotaka kugombea nafasi mbalimbali kuchukua fomu za kugombea;
(f) Tarehe na muda wa kuchukua na kurudisha fomu za maombi ya kugombea;
(g) Siku ambayo uteuzi utafanyika na sehemu ya matangazo ya Uchaguzi ambapo fomu za wagombea zitabandikwa;
(h) Muda wa kuweka pingamizi dhidi ya uteuzi na muda wa kusikilizwa kwa pingamizi;
(i) Tarehe ya kusikiliza rufaa dhidi ya uteuzi na kusikilizwa kwa pingamizi;
(j) Kipindi cha kuendesha mikutano ya kampeni za Uchaguzi; na
(k) Masuala mengine yanayohusu Uchaguzi.

6. Makosa ya Uchaguzi na Adhabu Zake

Kwa mujibu wa *kifungu cha 48 (Mamlaka za Wilaya -Vijiji* na *Mamlaka za Miji), na kifungu cha 45* (Mamlaka za Wilaya- Kitongoji) makosa ya kiUchaguzi ni:-

1. Kuharibu orodha ya wapiga kura au nyaraka zozote zinazohusiana na Uchaguzi.
2. Kutoa taarifa za uongo ili kupiga kura.
3. Kujiandikisha au kupiga kura zaidi ya mara moja.
4. Kutishia wapiga kura au wagombea ili kuvuruga Uchaguzi.
5. Kufanya kampeni siku ya Uchaguzi.
6. Kuonyesha ishara au kuvaa mavazi yanayoashiria kumtambulisha mgombea au chama cha siasa katika eneo la mita mia mbili kutoka kwenye kituo cha kupigia kura.
7. Kumzuia Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, Msimamizi wa Kituo, Mjumbe wa Kamati ya Rufaa au Afisa wa Umma aliyeteuliwa kusimamia Uchaguzi kutekeleza majukumu yake.
8. Kukiuka masharti ya kiapo chake.
9. Kupatikana na karatasi za kupiga kura zaidi ya moja kwa nafasi moja inayogombewa.
10. Kuvuruga ratiba ya mikutano ya kampeni za Uchaguzi au kuvunja masharti ya kampeni za Uchaguzi.
11. Kufanya jambo lolote kinyume na Kanuni hizi.
12. Kukutwa na silaha kinyume cha sheria kwenye eneo la uteuzi wa wagombea, mikutano ya kampeni, eneo la usikilizaji wa rufaa za wagombea, kituo cha kuandikisha wapiga kura au kituo cha kupiga na kuhesabu kura.
13. Kutangaza matokeo ya Uchaguzi kabla hayajatangazwa na Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi au Msimamizi wa Kituo kwa mujibu wa Kanuni hizi.

Mtu yeyote akithibitika kuwa na hatia ya makosa hayo atakuhukumiwa adhabu ya faini isiyozidi Shilingi laki tatu (300,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili (12) au vyote kwa pamoja.

Kanuni pia zinawataka Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, Msimamizi wa Kituo, Wajumbe wa Kamati ya Rufaa au Mtumishi wa Umma atakayeteuliwa kusimamia Uchaguzi kuzingatia Sheria, Kanuni, Maelekezo na Matangazo kama yatakavyotolewa kwa mujibu wa Kanuni hizi.

7. Uandikishaji wa Wapiga Kura

Kwa mujibu wa Kanuni hizi:-

1. Uandikishaji unapaswa kuanza siku 47 kabla ya tarehe ya kupiga Kura. Hivyo, uandikishaji utafanyika kuanzia tarehe **8 -14 Oktoba, 2019**.
2. Uandikishwaji unatakiwa kufanyika katika majengo ya umma na pale ambapo hakuna jengo la umma, uandikishwaji utafanyika kwenye sehemu ambayo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atakuwa amekubaliana na viongozi wa vyama vya siasa.
3. Kituo cha kuandikishia wapiga kura kinatakiwa kufunguliwa saa mbili kamili asubuhi (2:00) na kufungwa saa kumi na mbili kamili jioni (12:00).
4. Watendaji wa Vijiji na Kata hawatateuliwa wala hawataruhusiwa kuandikisha au kuandaa orodha ya wapiga kura.
5. Wakati wa uandikishaji, Vyama vya Siasa vinaweza kuweka wakala wake kwa kila kituo cha kuandikishia wapiga kura.
6. Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi anatakiwa kubandika nakala ya orodha ya wapiga kura siku moja baada ya kukamilika kwa uandikishaji wa wapiga kura, nakala halisi ataitunza.
7. Mkazi ambaye amejiandikisha ana haki ya kukagua orodha ya wapiga kura katika muda wa siku saba (7) tangu tarehe ya orodha hiyo kubandikwa sehemu ya matangazo kwa lengo la kuweka pingamizi kuhusu usahihi wa orodha hiyo au kuomba orodha hiyo irekebishwe kwa kuongeza jina lake, kubadilisha taarifa zilizo katika orodha hiyo au kufuta jina lililoorodheshwa kwa vile aliyeorodheshwa amefariki.

8. Sifa za Mpiga Kura

Mkazi yeyote atapiga kura endapo atakuwa na sifa zifuatazo:-

1. Awe ni raia wa Tanzania.
2. Ana umri wa miaka kumi na nane (18) au zaidi.
3. Awe ni mkazi wa eneo la Kitongoji, Kijiji au Mtaa husika.
4. Hana ugonjwa wa akili uliothibitishwa na Daktari anayetambulika na Serikali au Bodi ya Utabibu.
5. Awe amejiandikisha kupiga kura katika eneo husika.

9. Kupoteza Sifa za Kupiga Kura

1. Mtu hatakuwa na haki ya kupiga kura kama hana mojawapo ya sifa tano (5) zilizotajwa hapo awali.
2. Kama atakuwa amejiandikisha kupiga kura katika kituo zaidi ya kimoja.

10. Sifa za Mgombea

Mkazi yeyote wa Kitongoji, Kijiji au Mtaa anaweza kugombea Uenyekiti au Ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji au Ujumbe wa Kamati ya Mtaa endapo:

1. Ni raia wa Tanzania.
2. Ana umri wa miaka ishirini na moja (21) au zaidi.
3. Ana uwezo wa kusoma na kuandika Kiswahili au Kiingereza
4. Ana shughuli halali ya kumwezesha kuishi.
5. Ni mkazi wa Mtaa, Kijiji na Kitongoji wa eneo husika.
6. Ni mwanachama wa chama cha siasa na amedhaminiwa na chama hicho.
7. Hajawahi kupatikana na hatia kwa kosa la utovu wa uaminifu katika kipindi cha miaka mitano kabla ya terehe ya Uchaguzi.
8. Hana ugonjwa wa akili uliothibitishwa na Daktari anaetambulika na Serikali au Bodi ya Utabibu.



11. Mgombea Kupoteza Sifa

Mtu hatakuwa na sifa za kugombea nafasi ya Uenyekiti wa Kijiji, Uenyekiti wa Mtaa, Uenyekiti wa Kitongoji, Ujumbe wa Halmashauri au Ujumbe wa Kamati ya Mtaa endapo:-

1. Amepoteza au hana sifa za mgombea zilizoainishwa.
2. Amehukumiwa hukumu ya kifo na Mahakama za Tanzania au anatumikia kifungo cha zaidi ya miezi sita jela.
3. Ana mkataba au maslahi kwenye kampuni ambayo ina mkataba na mamlaka ya Serikali za Mitaa ambayo anagombea nafasi ya uongozi na hajatangaza kuwepo kwa mkataba au maslahi yake kupitia kwenye gazeti linalopatikana katika eneo husika au mbao za matangazo katika Ofisi ya Kijiji au Mtaa.
4. Amepoteza sifa ya kupiga kura chini ya Kanuni hizi au kwa mujibu wa sheria yoyote inayohusu makosa ya Uchaguzi.
5. Hatojaza fomu za tamko la kuheshimu taratibu za maadili.
6. Ataajiriwa au kuteuliwa katika wadhifa wowote katika utumishi wa umma au kuchaguliwa katika nafasi ya Udiwani, Ubunge, Uspika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Umakamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

12. Uteuzi wa Wagombea (kuchukua na kurejesha fomu)

Mtu anaekusudia kugombea nafasi yeyote katika Serikali ya Mtaa atapaswa kuchukua, kuijaza na kurejesha fomu ndani ya siku saba (7). Kwa Uchaguzi wa mwaka 2019 tarehe ya kuchukua fomu ni tarehe **29/10/2019 - 4/11/2019**.

Fomu za uteuzi za kugombea nafasi hizi zinatolewa na kurejeshwa na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kuanzia saa moja na nusu (1.30) asubuhi hadi saa kumi kamili (10.00) jioni. Baada ya saa kumi kamili (10.00) jion, siku ya mwisho ya kurejesha fomu, Msimamizi Msaidizi haruhusiwi kupokea fomu kutoka kwa mtu yeyote.

13. Mahali, Vituo na Muda wa Kupiga Kura

Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Mwenyekiti wa Kitongoji, Mwenyekiti wa Mtaa, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Wajumbe wa kamati ya Mtaa utafanyika katika Vitongoji na Mitaa husika. Kura zitapigiwa katika majengo ya umma. Kama hakuna majengo ya umma Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi atalazimika kushauriana na wagombea wa vyama vya siasa na kisha kuchagua eneo lingine la kupigia kura. Kura zitapigwa kuanzia saa mbili (2:00) asubuhi mpaka saa kumi (10:00) jioni.

Ikifika saa kumi jioni askari atasimama nyuma ya mtu wa mwisho kwenye mstari ili kuzuia waliochelewa wasipige kura. Masanduku ya kupigia kura yatawekwa mahali ambapo kila mpiga kura atafikia kiurahisi. Msimamizi Msaidizi atahakikisha watu wenye mahitaji maalumu watawezeshwa kupiga kura katika mazingira rafiki kwao.

14. Utambulisho wa Mpiga Kura

Jina la mpiga kura ni sharti liwe kwenye orodha ya wapiga kura. Na pia mpiga kura lazima awe na kitambulisho kimojawapo kati ya:-

1. Kitambulisho cha mpiga kura.
2. Kitambulisho cha kazi.
3. Hati ya kusafiria.
4. Kadi ya Bima ya Afya.
5. Kitambulisho cha shule au chuo.
6. Kitambulisho cha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.
7. Leseni ya udereva.
8. Kitambulisho cha Taifa.

Endapo mpiga kura hana kitambulisho chochote na jina lake limo kwenye orodha ya wapiga kura Msimamizi wa Kituo atamruhusu apige kura mara baada ya kutambuliwa na wakazi wa eneo hilo.

15. Siku ya Upigaji Kura

Kura zitapigwa kwa kuzingatia usiri, Viongozi watakaochaguliwa ni Mwenyekiti wa Kitongoji katika ngazi ya Kitongoji, Mwenyekiti na Wajumbe wa Halmashauri katika ngazi ya Kijiji na Mwenyekiti wa Mtaa na wajumbe wa kamati ya Mtaa katika ngazi ya Mtaa. Mara baada ya kupiga kura, mpiga kura atatakiwa kuchovya kidole cha mkono katika kidau cha wino.

Wakati wa kupiga kura watu wafuatao wataruhusiwa kushuhudia zoezi la upigaji kura:

1. Msimamizi wa Uchaguzi.
2. Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi.
3. Askari, au Afisa wa Polisi ama Mgambo mwenye sare au.
4. Afisa yoyote atakayesimamia ulinzi.
5. Wakala wa chama cha siasa chenye mgombea.
6. Mwangalizi wa Uchaguzi mwenye kitambulisho.

Mtu mwingine yeyote hataruhusiwa kubaki katika eneo la kituo cha kupigia kura mara baada ya kupiga kura.

16. Usaidizi kwa Watu wenye Mahitaji Maalum

Ili kuzingatia haki za watu wenye mahitaji maalumu mfano wenye Ulemavu, Kanuni zinamruhusu kuomba msaada wakati wa kupiga kura, isipokuwa mtu huyo asiwe Msimamizi ama Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi. Hata hivyo, mtu mmoja hataruhusiwa kumsaidia zaidi ya mpiga kura mmoja.



17. Kuhesabu Kura

Kura zitahesabiwa kwenye kituo cha kupigia kura na Msimamizi wa Kituo mbele ya wagombea au mawakala wao. Kabla ya kuhesabu kura Msimamizi wa Kituo atafanya mambo yafuatayo:

1. Atahakiki idadi ya wakazi waliopiga kura,
2. Atahesabu idadi ya karatasi za kupigia kura ambazo hazikutumika na kuziweka kwenye bahasha maalum.
3. Atakagua lakiri na kuona kama haijafunguliwa.
4. Atakata lakiri na.
5. Atafungua sanduku la kupigia kura na kuanza kuhesabu.

Wanaoruhusiwa kushuhudia zoezi la kuhesabu Kura ni:

1. Msimamizi wa Uchaguzi.
2. Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi.
3. Askari au Afisa Polisi.
4. Mgambo mwenye sare au Afisa yoyote atakaye simamia Uchaguzi.
5. Mwangalizi wa Uchaguzi mwenye kitambulisho.
6. Mgombea.
7. Wakala wa vyama vya Siasa.



18. Kutangazwa kwa Matokeo

Mgombea aliyepata kura nyingi ndiye atakayetangazwa kuwa mshindi kwa nafasi ya Mwenyekiti wa Kitongoji, Mwenyekiti wa Kijiji, Mwenyekiti wa Mtaa, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa. Matokeo yatabandikwa kwenye mbao za matangazo. Ikiwa idadi ya kura zilizopigwa zinalingana kwa watu waliogombea basi Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atapanga tarehe nyingine ya kurudia Uchaguzi huo ndani ya siku kumi na nne (14) tangu siku ya Uchaguzi.

19. Kutobatilisha Matokeo ya Uchaguzi

Masuala yafuatayo hayatabatilisha matokeo ya Uchaguzi ambayo ni:-

1. Kutokuwepo kwa Mgombea au Wakala wakati wa kupiga kura.
2. Kutokuwepo kwa Mgombea au Wakala wakati wa kuhesabu kura.
3. Kutokuwepo kwa Mgombea au Wakala wakati wa kutangaza matokeo na;
4. Mgombea au Wakala kukataa kusaini fomu ya matokeo.

20. Kampeni za Uchaguzi

Kwa mujibu wa Kanuni, kampeni za Uchaguzi zitafanyika **siku saba (7)** kabla ya siku ya Uchaguzi. Aidha, chama cha siasa kinachoshiriki Uchaguzi kitawasilisha ratiba ya mikutano ya kampeni kwa Msimamizi wa Uchaguzi siku saba (7) kabla ya kuanza kwa kampeni.

Baada ya kupokea ratiba za vyama vyote vya siasa vyenye wagombea na vyama kuridhia, Msimamizi atawasilisha ratiba hiyo kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya siku tatu (3) kabla ya kampeni kuanza.

21. Waangalizi wa Ndani wa Uchaguzi

Kwa mujibu wa Kanuni hizi Waangalizi wa ndani wa Uchaguzi wataweza kuangalia Uchaguzi baada ya kupata kibali kutoka kwa Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana ya Serikali za Mitaa ndani ya muda wa siku 21 baada ya Tangazo la Uchaguzi kutolewa.

Waangalizi wa ndani wa Uchaguzi watafanya shughuli za uangalizi kwa gharama zao wenyewe na watatakiwa kuzingatia masharti ya Kanuni hizi na Miongozo itakayotolewa ikiwa ni pamoja na kutoingilia kwa namna yoyote shughuli ya Uchaguzi.

22. Elimu ya Mpiga Kura na Uraia

Kwa mujibu wa Mwongozo wa Elimu ya Mpiga Kura kwa ajili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, 2019. Taasisi yoyote inayotaka kutoa elimu ya mpiga kura itapaswa kufanya maombi na kuwasilisha nyaraka zenye taarifa zifuatazo:

1. Cheti cha usajili.
2. Barua ya usajili kuthibitisha uhai wa Taasisi.
3. Katiba ya Taasisi.
4. Majina na anuani ya Viongozi wa Taasisi.
5. Namba za simu za taasisi /viongozi.
6. Anuani ya ofisi.
7. Taarifa ya fedha inayoonesha vyanzo vya fedha.
8. Taarifa za rasilimali watu na vitendea kazi katika utoaji elimu.
9. Vibali vya kazi kwa wasio raia wa Tanzania.
10. Taarifa nyingine yoyote itakayohitajika.

Gharama za kutoa elimu ya mpiga kura na uangalizi wa Uchaguzi zitakua jukumu la Taasisi husika, kutokana na kukosekana kwa Mwongozo kuhusu elimu ya uraia katika Kanuni hizi, utoaji wa elimu ya uraia utafanyika kwa mujibu wa Miongozo ya Kisheria na KiKanuni zinazoongoza utoaji wa elimu hiyo nchini Tanzania.

Maombi ya uangalizi wa Uchaguzi na utoaji wa elimu ya mpiga kura yatumwe kwa anuani:

Katibu Mkuu
Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI)
S.L.P 1923, Dodoma
Barua Pepe: ps@tamisemi.go.tz

Kiambatanisho 1: Kalenda ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2019

NA	TUKIO	MUDA	TAREHE
1	Waziri Kutoa tangazo la Uchaguzi wa Serikali za mitaa wa mwaka 2019	Siku 90 kabla ya siku ya Uchaguzi	23/08/2019
2	Kutolewa kwa tangazo la Uchaguzi kwenye magazeti ya kiswahli na kiingereza	Siku 90 kabla ya siku ya Uchaguzi	26/08/2019
3	Maombi ya kuangalia Uchaguzi	Siku 89 kabla ya siku ya Uchaguzi	27/8-16/9/2019
4	Uteuzi wa wasimamizi wa Uchaguzi	Siku 84 kabla ya siku ya Uchaguzi	2-9/9/2019
5	Kutolewa kwa tangazo la majina na mipaka ya vijiji, vitongoji na mitaa	Siku 72 kabla ya siku ya Uchaguzi	13/09/2019
6	Uteuzi wa wasimimazi wasaidizi wa Uchaguzi na wasimamizi wa vituo	Siku 69 kabla ya Uchaguzi	16-22/9/2019
7	Msimamizi wa Uchaguzi kutoa maelekezo ya Uchaguzi ikiwemo tarehe ya Uchaguzi	Siku 62 kabla ya siku ya Uchaguzi	23/09/2019
8	Uteuzi wa mwandikishaji wa wapiga kura. Msimamizi wa Uchaguzi atamteua Mtumishi wa Umma ambaye ataandikisha na kuandaa orodha ya wapiga kura	Siku 52 kabla ya siku ya Uchaguzi	3/10/2019
9	Uandikishaji wa wapiga kura utafanyika kwa siku 7	Siku 47 kabla ya siku ya Uchaguzi	8-14/10/2019
10	Kubandikwa kwa orodha ya wapiga kura	Siku 50 kabla ya siku ya Uchaguzi	15/10/2019
11	Ukaguzi wa orodha ya wapiga kura	Siku 50 kabla ya siku ya Uchaguzi	15-21/10/2019
12	Pingamizi kuhusu uandikishaji wa wapiga kura	Siku 50 kabla ya siku ya Uchaguzi	15-21/10/2019

13	Uamuzi kuhusu pingamizi ya wapiga kura	Siku 49 kabla ya siku ya Uchaguzi	21-22/10/2019
14	Marekebisho ya orodha ya wapiga kura	Siku 49 kabla ya siku ya Uchaguzi	21-22/10/2019
15	Kukata rufaa dhidi ya uamuzi wa pingamizi	Siku 49 kabla ya siku ya Uchaguzi	21-23/10/2019
16	Uamuzi wa rufaa	Siku 49 kabla ya siku ya Uchaguzi	21-26/10/2019
17	Ukomo wa kuwa madarakani	Siku 7 kabla ya siku ya kuchukua fomu	22/10/2019
18	Uteuzi wa kamati ya rufani	Siku 26 kabla ya siku ya Uchaguzi	29/10/2019
19	Kuchukua na kurudisha fomu za kugombea nafasi ya uenyekiti wa Kijiji na mitaa, ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji na mitaa au uenyekiti wa Kitongoji,	Siku 26 kabla ya Uchaguzi	29/10-4/11/2019
20	Uteuzi wa wagombea wa nafasi ya uenyekiti wa Kijiji na mitaa, ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji na mitaa na uenyekiti wa Kitongoji	Siku 19 kabla ya siku ya Uchaguzi kuanzia saa 2 kamili asubuhi hadi saa 10 kamili jioni	5/11/2019
21	Uwasilishaji wa pingamizi kuhusu uteuzi wa wagombea	Siku 19 kabla ya siku ya Uchaguzi	5-6/11/2019
22	Uamuzi wa pingamizi kuhusu uteuzi wa wagombea	Siku 19 kabla ya siku ya Uchaguzi	5-7/11/2019
23	Kutaka rufaa dhidi ya uamuzi wa kuhusu pingamizi la uteuzi	Siku 19 kabla ya siku ya Uchaguzi	5-8/11/2019
24	Uamuzi wa kamati ya rufaa	Siku 19 kabla ya siku ya Uchaguzi	5-9/11/2019
25	Uwasilishaji wa ratiba za mikutano ya kampeni kutoka katika vyama vya siasa	Siku 7 kabla ya kampeni	10/11/2019

26	Uwasilishaji wa ratiba za mikutano ya kampeni kwa mkuu wa polisi wa wilaya	Siku 3 kabla ya kampeni	14/11/2019
27	Kufanya kampeni	Siku 7 kabla ya siku ya Uchaguzi	17- 23/11/2019
28	Kupiga, kuhesabu kura na kutangaza matokeo	Saa 2 kamili mpaka saa 10 kamili jioni	24/11/2019

Washiriki wa Kikosi Kazi:

1. Kellen Mngoya – HAFOTA
2. Hebron Mwakagenda – The Leadership Forum
3. Israel Ilunde – YPC
4. Deus Kibamba – Tanzania Citizens' Information Bureau/Ushiriki Tanzania
5. Goodluck William Minja – UNA Tanzania
6. William Mtwazi – LHRC
7. Rehema Maro – WILDAF/Ushiriki Tanzania
8. Jimmy Luhende – Actions for Democracy and Local Governance (ADLG)
9. Richard Angelo – Policy Forum Sekretarieti
10. Farida Kiobya – Policy Forum Sekretarieti
11. Rashid Kulewa – Policy Forum Sekretarieti

Kwa maoni na ushauri wa kijitabu hiki, waweza kuwasiliana na Policy Forum: Nyumba Na: 14, Mtaa wa Sembeti, Barabara ya Mwai Kibaki, Mikocheni B, S.L.P 38486, Dar es Salaam, Tanzania Simu: +255 22 2780200, Simu ya Kiganjani: +255 782 317434 Barua pepe: info@policyforum.or.tz, Tovuti: www.policyforum-tz.org

Justice Lugakingira House, Kijitonyama
S.L.P 75254, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255222773038/48
Nukushi: +255222773037
Barua pepe: lhrc@humanrights.or.tz
Tovuti: www.humanrights.or.tz

Nyumba Na: 14, Mtaa wa Sembeti
Barabara ya Mwai Kibaki | Mikocheni B
S.L.P 38486, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2780200
Simu ya Kiganjani: +255 782 317434
Barua pepe: info@policyforum.or.tz
Tovuti: www.policyforum-tz.org

@policy_F @policy_forum @policyforum1 @ PolicyForumTZ